Ufalame Wa Mbinguni

(The Kingdom of Heaven)

Na

Ellis P. Forsman

Ufalame Wa Mbinguni

(The Kingdom of Heaven)

Na

Ellis P. Forsman

October 15, 2011

Ufalme Wa Mbinguni

Mat. 13:11

"*Maudhui" ya jumla katika mfano huu wa Yesu ulikuwa ni "ufalme wa mbinguni*".

Mifano mingi huanza na "Ufalme wa mbingni unafanana na…"

- Mat. 13:24, "*Akawatolea mfano mwingine akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake;*"
- Mat. 13:31, "*Akawatolea mfano mwingine akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na punje ya haradali, aliyoitwaa mtu akaipanda katika shamba lake;*"
- Mat. 13:33, "*Akawaambia mfano mwingine, Ufalme wa mbinguni umefanana na chachu aliyoitwaa mwanamke akaisitiri ndani ya pishi tatu za unga hata ukachachwa wote pia.*"
- Mat. 13:44-45, "*Tena ufalme wa mbinguni umefanana na hazina iliyositirika katika shamba ambayo mtu alipoiona aliificha; na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote akalinunua shamba lile. Tena ufalme wa mbinguni umefanana na mfanya biashara mwenye kutafuta lulu nzuri;*"
- Mat. 13:47, "*Tena ufalme wa mbinguni umefanana na juya, lililotupwa baharini likakusanya samaki wa kila namna;*"

Katika kufafanua ni kwa nini aliongea kwa mifano, Yesu alielezea "*siri za ufalme wa mbinguni*". Mat. 13:11, "*Akajibu akawaambia ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa.*"

Pia tunaona kwamba, "*ufalme wa mbinguni*" ulikuwa ni maudhui ya…

Huduma ya safari za Yesu.

- Mat. 4:17, "*Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.*"
- Mat. 4:23, "*Naye alikuwa akizungumza katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari njema ya ufalme na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu.*"

Hotuba yake mlimani.

- Mat. 5:3, "*Heri walio masikini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao.*"
- Mat. 5:10, "*Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; maana ufalme wa mbinguni ni wao.*"
- Mat. 5:19-20, "*Basi mtu yeyote atakaevynja amri moja katika hizi zilizo ndogo na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni, bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni. Maana nawambia ya kwamba, haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.*"
- Mat. 5:33, "*Tena mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, usiape uongo ila mtimizie Bwana nyapo zako;*"
- Mat. 6:10, "*Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni.*"
- Mat. 7:21, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye wa mbinguni.*"

Kwa sababu "*ufalme wa mbinguni*" ni somo lililozoeleka katika mifano ya Yesu (pamoja na mafundisho yake kiujumla)…

Inaweza kuwa vyema kama tukiweka somo letu la mifano kwa mtazamo wa uangalifu wa kile ambacho "*ufalme wa mbinguni*" inamanisha.

Kwa fafanuzi sahihi ya "*ufalme wa mbinguni*" upya katika akili zetu, tunaweza kufaidika katika mafundisho ya Bwana wetu katika somo hili zuri!

Tuanze juhudi zetu kwa kufafanua "*ufalme wa mbinguni*" kwa kuilinganisha na "*ufalme wa mbinguni*".

"*ufalme wa mbinguni*" dhid ya "*ufalme wa mbinguni*"

Kuna tofauti?

Kuna baadhi ya watu wanao jaribu kuweka utofauti, lakini ulinganifu wa haraka wa injili unaonyesha kwamba matamshi haya humanisha kitu kile kile.

- Mat. 4:17 na Marko 1:14-15.
- Mat. 4:17, "*Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema tubuni maana ufalme wa mbinguni umekaribia.*"

- Marko 1:14-15, "*Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya akiihubiri habari njema ya Mungu, akisema wakati umetimia na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuamini injili.*"
- Mat. 5:3 na Luka 6:20.
- Mat. 5:3, "*Heri walio maskini war oho; maana ufalme wa mbinguni ni wao.*"
- Luka 6:20, "*Akainua macho yake akawatazama wanafunzi wake, akasema heri ninyi mlio maskini kwa sababu ufalme wa Mungu ni wenu.*"
- Mat. 13:31 na Marko 4:30-31.
- Mat. 13:31, "*Akawatolea mfano mwingine akisema, ufalme wa mbinguni umefanana na punje ya haradali, aliyoitwaa mtu akaipandaa katika shamba lake.*"
- Marko 4:30-31, "*Akasema tulinganishe na nini ufalme wa Mungu? Au tuutie katika mfano gani? Ni kama punje ya haradali, ambayo ipandwapo katika nchi, ingawa ni ndogo kuliko mbegu zote zilizo katika nchi,lakini ikiisha kupandwa hukua, ingawa kubwa kuliko miti yote ya mboga, ikafanya matawi makubwa, hata ndege wa angani waweza kukaa chini ya uvuli wake.*"

Kwa nini utofauti unaelezwa?

Tunakuta kwamba Mathayo alitumia maelezo "*ufalme wa mbinguni*" karibia isijumlishwe, wakati waandishi wengine wa vitabu vya injili walitumia neno "*ufalme wa Mungu*".

Inawezekana kwamba toka Mathayo alipoandika injili yake kwa Wayahudi, alichagua kutumia neno "*ufalme wa mbinguni*" kwa sababu ya uelewa mbovu wa Wayahudi kuhusu kuja kwa ufalme.

Wengi walidhani ni ufalme wa kimwili.

Neno "*mbingu*" (halisi, "*mbingu*") inasisitiza ufalme wa kiroho.

Hivyo uchunguzi wetu wa kwanza ni kwamba juhudi zozote za kutofautisha kati ya "*ufalme wa mbinguni*" na "*ufalme wa Mungu*" hakika haina uhalali.

Sasa tuangalie Yesu alimanisha nini alipoongelea "*ufalme wa mbingu*".

Inajumuisha maingiliano manne ya mawazo

Mungu anatawala.

Ni ya kiroho kiualisia; leo inaonyeshwa kwa kuonekana leo katika kanisa la Bwana; na inaelezwa kwamba uliopo na ujao.

Neno "*ufalme*" kama ilivyotumiwa na Wayahudi mara zote ilionyesha wazo la "utawala" 'miliki", siyo sehemu za kijiografia inayozunguka mazingira ya kimwili.

Imetumiwa kwa njia hii na Yesu katika Mat. 6:10.

Mat. 6:10, "Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni."

Hivyo, "*ufalme wa mbinguni*" (au "*ufalme wa Mungu*") ni popote ambapo "utawala" au "miliki" ya Mungu (aliye mbinguni) huonyeshwa.

Katika mtazamo mmoja, ufalme wa Mungu umekuwako siku zote.

- Zab. 47:2, "*Kwa kuwa BWANA aliyejuu, mwenye kuogofya, ndiye mfalme mkuu juu ya dunia yote.*"
- Zab. 103:19, "*BWANA ameweka kiti chake cha enzi mbinguni, na ufalme wake unavitawala vitu vyote.*"

Lakini katika njia maalum utawala au umiliki wa Mungu ulipaswa kuonyeshwa kwa kuja kwa Kristo.

Kama ilivyotabiriwa hapo awali katika kipindi cha Danieli (~500 B.C.).

Dan. 2:44-45, "*Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja ufalme hizi vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele. Na kama vile ulivyoona na kuwa jiwe lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono, nay a kuwa lilivunja vunja kile chuma, na ile shaba, na ule udongo, na ile fedha, na ile dhahabu; basi Mungu aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayo kuwa baadaye; na ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti.*"

Kama ilivyotangazwa na Yohana Mbatizaji.

Mat. 3:1-3, "*Siku zile aliondoka Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema, tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake.*"

Kama ilivyohubiriwa na Yesu.

- Mat. 4:17, "*Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.*"
- Marko 1:14-15, "*Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya akihubiri habari njema ya Mungu, akisema wakati umetimia na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuiamini injili.*"

Hakika, ni katika utu wa Yesu Kristo kwamba "*utawala wa Mungu*" huonyeshwa leo.

- 1 Kor. 15:23-26, "*Lakini kila mmoja mahali pake limbuko ni Kristo; baadae walio wake Kristo atakapokuja. Hapo ndipo mwisho atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu. Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti.*"
- Efe. 1:20-22, "*Aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu war oho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*"
- 1 Pet. 3:22, "*Naye yupo mkono wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini ya miguu yake.*"
- Ufu. 1:5, "*Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliyemwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake,*"

Ni ya kiroho katika ualisia.

Ufalme (au utawala wa Mungu) usingepatikana katika mfumo wa ufalme wa kimwili.

Yohana 18:36, "*Yesu akajibu ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa.*"

Itajidhiirisha yenyewe katika njia za kiroho.

Rum. 14:17, "*Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu.*"

Udhihirishwa kwa kuonekana leo katika kanisa la Bwana.

Kanisa la Bwana ni nini?

Ni jamii ya nafsi ambao katika roho zao Mungu utambulika kama mwenye Enzi yote.

Kwamba neno "*kanisa*" na "*ufalme*" zinaweza kutumika kwa kubadilishana, zingatia:

Jinsi "*kanisa*" na "*ufalme*" zilivyotumiwa na Yesu.

Mat. 16:18, "*Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*"

Maneno yaliyosemwa na wale waliokuwa ndani ya kanisa.

- Kol. 1:13, "*Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza na kutuingiza katika upya wa Mwana wa pendo lake.*"
- 1 Thes. 2:12, "*Ili mwenende kama ilivyo wajibu wenu kwa Mungu, mwenye kuwaita ninyi ili mwingie katika ufalme wake na utukufu wake.*"

Maelezo ya wale walikuwa ndani ya makanisa ya Asia.

- Ufu. 1:4, "*Yohana kwa yale makanisa saba ya Asia; neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwake yeye aliyeko na atakayekuwako na atakayekuja; na zitokazo kwa roho saba walioko mbele ya kiti chake cha enzi.*"
- Ufu. 1:6, "*Na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una yeye hata milele na milele. Amina.*"

- Ufu. 1:9, "*Mimi Yohana ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu.*"

Inaelezwa kuwa katika wakati uliopo na utakaokuja.

"*Ufalme wa mbinguni*" una ishara sawa na hii iliyopo.

Matokeo yake yajayo yanaongelewa na:

Yesu.

Mat. 25:34, "Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, njooni, mliobarikiwa na Baba yangu urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu;"

Paulo

- 1 Kor. 15:50, "*Ndugu zangu nisemayo ni haya, ya kuwa nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu, wala uharibifu kuurithi kutokuharibika.*"
- 2 Tim. 4:18, "*Bwana ataniokoa na kila neno baya na kunihifadhi hata nifike ufalme wake wa mbinguni. Utukufu una yeye milele na milele. Amina.*"

Petro.

2 Pet. 1:10-11, "*Kwa hiyo ndugu zangu jitahidini sana kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo.*"

Petro ameeleza hali ya wakati wa kuja kwake.

2 Pet. 3: 10-13, "*Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea. Basi kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa, hivyo imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gania katika mwenendo mtakatifu na utauwa, mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza; ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua na viumbe vya asili vitateketea na*

kuyeyuka? Lakini kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake."

Hivyo, "*ufalme wa mbinguni*" unajumuisha "*mbingu na nchi mpya*".

Mitazamo hii mine au kanuni lazima ziwekwe akilini kila tunapofikiria "*ufalme wa mbinguni*". Kushindwa kukumbuka zote nne itatuongoza kirahisi katika upotofu kuhusu uasili wa ufalme.

Katika juhudi za kuweka somo hili wazi hata zaidi, zingatia…

Tafsiri fupi ya "*ufalme wa mbinguni*"

Katika fikra ya wakati uliopo.

Inaapatikana kila ambapo utawala wa Mungu unakubaliwa katika mioyo ya wanadamu. Ni ufalme wa kiroho, kwa maana Mungu anatawala katika roho za wanadamu. Ni uonyesho wan je leo katika kanisa la Bwana.

Ufalme ulizinduliwa Siku ya Pentekoste kama ilivyonakiliwa kaatika Matendo ya Mitume.

Mdo. 3:36, "*Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo.*"

Katika mtazamo ujao.

Ufalme utafikia kiwango chake cha juu kwa kuja kwake Bwana.

- 1 Kor. 15:24, "*Hapo ndipo mwisho atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote na mamlaka yote, na nguvu.*"
- Mat. 13:43, "*Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenye masikio na asikie.*"

Itakuwa kwamba "*mbingu mpya na nchi mpya*" inaelezwa na Paulo na Yohana.

- 2 Pet. 3:13, "*Lakini kama ilivyo ahadi yake mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake.*"
- Ufu. 21:3, "*Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema tazama maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.*"

Itaonjwa tu na wale walioko ndani ya kanisa wanaojiweka katika mapenzi ya Mungu.

Kwa wale "*wanaofanya mapenzi ya Baba yangu aliyembinguni*".

Mat. 7:21-23, "*Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.*"

Wale "*walio na juhudi kukutwa naye katika amani*"

2 Pet. 3:13-15, "*Lakini kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake. Kwa hiyo wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika imani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake. Nanyi uhesabuni uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu, kama vile na ndugu yetu Paulo alivyowaandikia kwa hekima aliyopewa,*"

Hitimisho

Tunapoingia katika mifano ya Yesu, tutapata maelezo mengi kuhusiana na "*ufalme wa mbinguni*".

Wakati mwingine inatokea Yesu anaongelea mwonekano wa ufalme "uliopo". Kwa wakati mwingine anaongelea mwonekano "ujao" wa ufalme.

Natumai, juhudi hii ya kufafanua "*ufalme wa mbinguni*" utatusaidia kushukuru zaidi ambacho Yesu anapaswa kusema kuhusiana na "*siri za ufalme wa mbinguni*"!

Mfumo mmoja kuhusu kuingia katika ufalme ambao ulikuwa siri kwa Nikodemo mwanzoni ilikuwa ni hitaji la kuzaliwa kwa mara ya pili. Alafu Yesu anaeleza kwamba uzao mpya ulikuwa wa maji na Roho.

Yohana 3:3-5, "*Yesu akajibu akamwambia, Amin, amini, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa mara ya pili hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, amin, amini, nakuambia mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*"

Je hiyo bado ni siri kwako? Alafu zingatia Mdo. 2:38 na Tito 3:5.

- Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo,mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

- Tito 3:5, "*Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;*"